

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



19 MEI, 2016



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA ISHIRINI NA TATU – TAREHE 19 MEI, 2016

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

MWENYEKITI WA KAMATI YA NISHATI NA MADINI:

Taarifa ya Kamati ya Nishati na Madini kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 pamoja na Maoni ya Kamati juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI JUU YA WIZARA YA NISHATI NA MADINI:

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani juu ya Wizara ya Nishati na Madini kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

II. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:

III. MASWALI YA KAWAIDA:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

194. MHESHIMIWA HAWA MCHAFU CHAKOMA (VITI MAALUM):


Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Utekelezaji wa Maagizo ya Serikali Kuu kwa Halmashauri imekuwa ni changamoto na mzigo mkubwa kwa Halmashauri hizo hususan Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha ambapo maagizo mengi hayamo kwenye mpango wa Bajeti na hivyo utekelezaji unakuwa mgumu:-

Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha maagizo hayo yanatengewa Bajeti.

WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

195. MHESHIMIWA PETER AMBROSE LIJUALIKALI (KILOMBERO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Wilaya ya Kilombero ni moja kati ya Wilaya zinazozalisha kwa wingi mazao ya chakula lakini barabara zake nyingi ni mbovu na hivyo kushindwa kusafirisha mazao kwa urahisi:-

- 
- (a) Je, ni lini barabara ya Kidatu - Ifakara na Ifakara - Mlimba itajengwa kwa kiwango cha lami;
 - (b) Je, ni lini daraja la Mto Kilombero linalouunganisha Wilaya za Kilombero, Malinyi na Ulanga litamalizika.

196. MHESHIMIWA NJALU DAUDI SILANGA (ITILIMA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Mkandarasi katika Barabara ya kutoka Mweguasi - Maswa tayari ameshapatikana na yuko eneo la kazi:-

Je, ni lini barabara ya kutoka Maswa – Itilima – Bariadi itapatiwa Mkandarasi kwa ajili ya kuunganisha kipande hicho cha barabara.

WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:

197. MHESHIMIWA MAFTAH ABDALLAH NACHUMA (MTWARA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Miundombinu ya maji Mtwara na Mikoa yote ya Kusini mwa Tanzania ni hafifu na wakazi wengi wa Miji ya Kusini na Vijiji hawapati maji safi na salama:-

Je, Serikali iko tayari kujenga bomba la kuvuta maji toka Ruvuma ambalo limekuwa likizungumziwa kwa muda mrefu bila mafanikio.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI:

198. MHESHIMIWA FAKHARIA SHOMAR KHAMIS (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani:- Magari yanayobeba abiria nchini yamekuwa yakitozwa faini pindi yanapokamatwa kwa kosa la kujaza abiria zaidi ya uwezo wake badala ya kutakiwa kupunguza abiria waliozidi:-

- (a) Je, Serikali haioni kuwa kutoza faini na kuacha gari liendelee na safari huku likiwa limejaza ni sawa na kuhalalisha kosa;
- (b) Je, Serikali haioni kuwa ikiwashusha abiria waliozidi itakuwa imetoa fundisho na kupunguza ajali kwa abiria ambao hupanda gari huku wakijua limejaa.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:

Kwamba, Bunge sasa likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

DODOMA
19 MEI, 2016

DKT. T. D. KASHILILAH
KATIBU WA BUNGE

